# Kiswahili nchini Kenya: ukuaji au ukiushi?

**C. Momanyi**
*Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta*

**Ikisiri**
Makala hii inadondoa baadhi ya mifano ya miundo ya maneno pamoja na uvunjaji wa mfuatano wa kisarufi unaobainika katika baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Makala inahoji kama haya ni maendeleo ya lugha au ni njia mojawapo ya kuidumaza isiweze kuchukua nafasi yake kama lugha ya taifa nchini. Katika sehemu ya mwisho ya makala, yanatolewa mapendekezo ambayo yamekusudiwa kusahihisha hali iliyopo ili kukifanya Kiswahili kama lugha muhimu nchini Kenya, iweze kujitanua kimatumizi na kurejesha hadhi yake kama lugha ya walio wengi nchini humo.

## 1.0 Utangulizi

Kiswahili kama lugha nyingine yoyote ulimwenguni ina uwezo wa kujitanua na kujiendeleza kimsamiati. Hata hivyo, ieleweke kwamba hakuna lugha ulimwenguni inayoweza kueleza kila kitu, au inayoweza kukidhi mahitaji ya wanadamu wote bila kutindikiwa kimsamiati. Hii ni kwa sababu kuna dhana zingine ulimwenguni ambazo lugha fulani haiwezi kuzieleza kutokana na sababu kuwa haijaenea kote ulimwenguni. Kwa kadri lugha inavyoenea na kukabiliana na mazingira na dhana mpya, ndivyo inavyobadilika na kujitanua kimsamiati.

Lugha ya Kiswahili imevinjari sehemu nyingi ulimwenguni kama chombo muhimu cha mawasiliano. Mbali na kwamba inazungumzwa katika nchi nyingi barani Afrika, imevuka bahari kuu ulimwenguni na kunawiri katika nchi kama vile Ujerumani, Ufaransa, Marekani, Urusi, Uchina, Uarabuni hata Korea Kusini. Inakisiwa kwamba lugha hii inazungumzwa na watu wanaozidi milioni 110 kote ulimwenguni (Kiswahili BBC, 1995). Bila shaka, idadi hii imeongezeka maradufu. Aidha, Massamba na wengineo (2001:2) wanaeleza kwamba lugha hii hutumiwa na watu zaidi ya takriban milioni 60. Takwimu hizi zinabainisha kwamba lugha hii inatajika katika safu za kimataifa kama chombo aali cha mawasiliano.

Lugha hutumiwa kama ishara ya kuifasiria mifumo na miktadha ya kijamii na kiutamaduni (Halliday, 1978). Hata hivyo, lugha kama utaratibu wa kiishara haina budi kufuata kanuni fulani za uundaji wa maneno, kanuni zinazokubalika miongoni mwa waneni wake. Nchini Kenya, Kiswahili kilipata msukumo na pumzi mpya wakati serikali ilipoanzisha mfumo wa elimu ya 8.4.4 kwenye mwaka wa 1985. Hatua hii iliwapa waalimu ilhamu ya kuikuza lugha hii, na wanafunzi wakajikakamua vilivyo ili kujifunza lugha iliyokuwa imesahauliwa katika safu za kielimu.

Jambo linaloshangaza wengi hivi sasa ni mwelekeo ambao lugha hii inachukua. Ijapokuwa jamii huweza kupambanuliwa kutokana na njia zake mbalimbali za kuzungumza, baadhi ya watumiaji wa Kiswahili nchini Kenya wameibua njia potovu za kuzungumza. Njia hizi zinavurujua maneno kiasi cha kuvunjilia mbali kanuni za uundaji wa maneno katika lugha hii.

Makala hii inadondoa baadhi ya mifano ya miundo ya maneno pamoja na uvunjaji wa mfuatano wa kisarufi unaobainika katika baadhi ya waneni wa lugha hii. Makala inasaili iwapo haya ni maendeleo ya lugha au ni njia mojawapo ya kuidumaza isiweze kuchukua nafasi yake kama lugha ya taifa nchini. Mwisho bali si akali, makala inatoa mapendekezo ambayo kwayo Kiswahili kama lugha muhimu nchini Kenya, inaweza kujitanua kimatumizi na kurejesha hadhi yake kama lugha ya wengi nchini.

## 1.1 Matumizi ya Kiswahili nchini Kenya

Kiswahili kama lugha mojawapo muhimu ya mawasialiano nchini Kenya, imepitia kwenye njia tata zenye uwezo wa kuibananga isiweze kujitanua katika asasi mbalimbali za jamii. Hata hivyo, lugha hii imeendelea kupiga hatua kulingana na jinsi waneni wake wanavyoendelea kuikuza kupitia njia mbalimbali. Baadhi ya njia hizi ni kama vile ukopaji wa maneno kutoka katika lugha zingine. Dhana mpya zinazoingizwa katika jamii lazima zitafutiwe msamiati. Hata hivyo, ni kawaida maneno ya mkopo kutoka kwa lugha mnamopatikana dhana hizo yakaingizwa moja kwa moja katika lugha pokezi. Msamiati wa kiteknolojia huweza kutumiwa kueleza dhana au vitu vinavyohusiana na teknolojia za kigeni zinazoingizwa kutoka nje. Aidha, lugha ya Kiswahili inaendelezwa kupitia ufasiri wa maana. Hapa neno huundwa kutokana na maana mbili tofauti ambapo neno lenye maana changamano hupatikana. Maneno kama haya huwa yamefanyiwa uhuluti. Mfano mahsusi ni ule wa neno ukimwi, ambalo liliundwa kutokana na maneno matatu (<u>U</u>kosefu wa <u>Ki</u>nga <u>Mwi</u>lini).

Mbinu ya tafsiri ya moja kwa moja pia imetumiwa ili kuirutubisha lugha hii kutokana na dhana au vitu vinavyoingizwa katika jamii-lugha, na ambavyo havina budi kutafsiriwa. Ifahamike pia kwamba maendeleo ya haraka katika nyanja mbalimbali za maarifa ya binadamu ndiyo yanayolazimisha kuundwa kwa dhana mpya au pia kubadilika kwa dhana zilizoko. Kila wakati, binadamu amekuwa akibuni dhana mpya ambazo zinahitaji kupewa maumbo ya kiisimu. Kama anavyoeleza Kwesi Prah (1993) ni kwamba kila lugha ina ufunguo ambao waneni wake huutumia kufungulia maana na urithi wa utamaduni mahsusi ambao lugha hiyo imefumwa. Kwa hivyo, anaendelea kueleza Prah, lugha ni vifurushi mahsusi vya kitamaduni vilivyosheheni historia za jamii husika. Pengine hii ndiyo maana inayowafanya wataalamu wa lugha kueleza kuwa lugha ni kioo ambacho kwacho tunaweza kuufasiri na kuuhakiki utamaduni wa jamii fulani.

Tunaporejelea nchi ya Kenya, tunaweza kuona kwamba mkondo wa maendeleo ya Kiswahili unatuelekeza mahali penye utata mwingi, na kwa hivyo kuyumbisha ufanisi na hadhi yake nchini. Hili ni daro kubwa linalowakabili wasomi na watafiti wa lugha hii kwani Kiswahili sasa kimefika kwenye njia panda. Wanaojifunza lugha hii, hasa wageni, hawajui washike njia gani. Ukopaji wa maneno ni njia mojawapo iliyodokezwa hapo juu kuwa imetumiwa ili kukuza Kiswahili. Hata hivyo, kiwango cha ukopaji wa maneno hasa ya Kiingereza ni cha kushangaza. Hii ni kwa sababu hatuoni ukopaji na uswahilishaji wa maneno

ya mkopo tuu, bali tunashuhudia kuvunjwavunjwa kwa mofimu za Kiingereza na Kiswahili pale zinapotumiwa pamoja ili kuunda neno.

Hali hii inabainika zaidi hasa miongoni mwa vijana, lakini pia miongoni mwa wanasiasa, hata waalimu. Kwa mfano, miongoni mwa vijana kumezuka namna fulani ya uzungumzi. Nimeiita "namna" ya uzungumzi kwa sababu "Sheng" haiwezi kuwa lugha. Haina utaratibu mahsusi wa uundaji wa maneno wala haina utaratibu maalum wa kisarufi. Haiwezi pia kuwa msimbo kwa sababu hubadilikabadilika kila uchao, haina sura maalumu. Isitoshe, siku hizi msamiati unaoundwa hauchukui maneno ya Kiingereza na Kiswahili pekee kama ilivyokuwa hapo awali. Maneno mengi ya lugha lukuki za kikabila zilizomo nchini yameshehenezwa katika hazina ya msamiati wa "Sheng" na kuifanya iwe na utata mwingi (Momanyi 1998:18). Ni vigumu kupambanua utaratibu wake wa kimofolojia au wa kisintaksia.

Mbali na "Sheng", tatizo kubwa zaidi ni lile la uvunjaji wa mofimu za Kiingereza na Kiswahili miongoni mwa watu mbalimbali. Kwenye mihadhara ya kisiasa, wanasiasa huihasi lugha bila kujali mustakabali wake kwa vizazi vijavyo. Kwa mfano, utasikia wanasiasa wakitamka maneno kama *kum-kampenia, ku-elect viongozi, kubribe, ame-defect, kum-explainia*, na kadhalika.

Ajabu ni kwamba namna hii ya kuongea huendelezwa kwenye hadhira za watu, baadhi wakiwa hata hawajaenda shule, wala hawajui Kiingereza. Kuna baadhi ya waalimu ambao kutokana na athari za maongezi ya aina hii, hujikuta wakiendeleza uzungumzi huu katika madarasa yao.

Hali hii haitokani na upungufu wa Kiswahili, bali ni ukosefu wa uzingativu wa nidhamu bora katika maongezi. Hali hii sasa inaathiri kizazi kipya cha watoto ambao wamejikuta katika vurugu hili. Mnamo mwaka wa 1969, rais wa Kenya marehemu mzee Jomo Kenyatta alitoa kauli kwamba lugha ya Kiswahili ilifaa kutumiwa kama lugha rasmi nchini. Kwa vyovyote vile, hakusema kwamba Wakenya walikuwa na uhuru wa kuivuruga lugha hii kiasi cha kukaribia kuwa na "chapa" ya Kiswahili. Kwa kadri tunavyokopa bila mpango msamiati wa kigeni, ndivyo tunavyozidi kuvunjilia mbali sintaksia na mofolojia ya lugha hii.

Kuhusu ukopaji wa maneno pia, wataalamu mbalimbali wametoa tahadhari dhidi ya mbinu hii ya kukuza lugha. Kwa mfano, Besha (1972:23) alieleza kwamba si lazima lugha ichukue maneno ya kigeni kila mara kunapokuwa na jambo jipya la kueleza. Alipendekeza kuwa maneno yenyewe ya lugha yanaweza kupanuliwa. Nkwera (1978) anakubaliana na hoja hii hasa anapoeleza kwamba chimbuko la msamiati katika uundaji wa msamiati wa Kiswahili linapasa kutokana na Waswahili wenyewe, yaani katika lahaja zake au katika makabila mengine ya Kibantu. Hatua hii ni bora kuliko kukimbilia lugha za kigeni. Nabhany (1978) ameonyesha dhahiri mtazamo huu kwa vitendo, kupitia uundaji wa baadhi ya maneno kwa kuzingatia "machimbo" ya msamiati wa kale wa Kiswahili.

Kutokana na kauli hizi, ni bayana kwamba ukopaji na *uswahilishaji* wa maneno ya mkopo hautakuwepo iwapo tungechukua muda kutafiti katika lahaja au ndimi asilia za Kiswahili ili kuteua msamiati katika mazingira mlimozaliwa lugha hii. Kwa sababu Kiswahili ni lugha ya Kiafrika iliyoinukia katika mazingira ya

Kiafrika, ingekuwa bora iwapo maendeleo ya kiistilahi na kimsamiati yangetazamwa katika muktadha wa Kiafrika. Hali inayobainika sasa nchini Kenya siyo ya ukopaji pekee, bali ni jaribio la kuidumaza zaidi lugha hii. Ukopaji si hoja kwani hata lugha zingine za kimataifa kama vile Kiingereza, zimekuzwa kwa njia hii. Kama asemavyo Massamba na wengine (2001:5), lugha kuwa na maneno mengi ya mkopo kutoka lugha nyingine peke yake hakuifanyi lugha hiyo isemekane kuwa imetokana na hiyo lugha nyingine. Wanasema jambo la muhimu kuzingatia ni muundo wa lugha kifonolojia, kimofolojia, kimsamiati na kisintaksia. Ninaafikiana na mawazo haya kwa sababu mifano ya maneno niliyodondoa hapo juu inaathiri vibaya kanuni za lugha ya Kiswahili.

Kila lugha, ikiwemo lugha ya Kiswahili, ina utaratibu wake wa uundaji maneno. Kwa mfano, katika uundaji wa majina au nomino, lugha hii huwa na viambishi vinavyotumiwa ili kubainisha hali ya umoja na wingi

| Kwa mfano: | umoja | wingi |
|---|---|---|
| | ki-chochoro | vi-chochoro |
| | m-temi | wa-temi |
| | m-gonjwa | wa-gonjwa |

Katika mifano hii, neno la mwisho hapa hutumiwa kimakosa na baadhi ya watu. Hii ni kwa sababu tunapotazama umbo-neno au mofolojia ya uundaji wa neno hili, tunakuta kwamba mzizi wake ni –gonjwa. Kwa kawaida, mzizi wa neno haubadiliki. Makosa yanayotokea ni kule kuuvunja mzizi wa neno ili uafiki matamshi yanayodhaniwa kuwa sahihi. Kwa mfano, kuna mazoea ya kutamka maneno kama *amegonjeka, kugonjeka*, au katika sentensi kama vile; *Jana niligonjeka sana*. Neno hili huwekwa katika kauli ya kutendeka kimakosa, kufuatia ule utaratibu wa kauli sahihi kama vile;

jenga – jengeka
kujenga – kujengeka

Makosa haya yameshika kasi nchini kiasi cha kuathiri hata watoto wa shule. Jambo la kushangaza pia ni kwamba hata wale wasiotarajiwa kufanya makosa kama hayo, kama vile waalimu wa Kiswahili, utawaona wakiyafanya bila kujali athari za baadaye, hasa kwa wanafunzi wao.

Kosa jingine linalobainika na kutawala mazungumzo ya wengi nchini, ni lile linalohusiana na vitenzi vyenye viini vya herufi moja. Hivi ni kama vile -pa, -fa, -la, na kadhalika. Vitenzi hivi ni vya viini vya herufi moja kwa sababu tukiondoa kiambishi tamati -a, tunabaki na herufi moja:

- p - a (ku-pa)
- l - a (ku - la)
- f – a (ku - fa )

Tunaponyambua vitenzi hivi, irabu hiyo ya – a, hupotea. Kwa mfano:

ku - peana (kupeana vitu).
ku - lia (kulia sahanini)

ku - fia (kufia mbali)

Neno linalotumiwa kimakosa hapa ni ku-pa. Vitenzi vinavyopatikana katika kitenzi hiki ni kama vile *mpe, pewa, nipe, nimempa tumepeana*, na kadhalika. Neno hili linatumiwa kimakosa kama vile: *amempea, mpee / nipee, peanwa na peana.* Kutokana na maneno haya, utasikia sentensi kama vile;

1. *Amempea mtoto chakula* badala ya *Amempa mtoto chakula*
2. *Nipee vitu zangu* badala ya *Nipe vitu vyangu*
3. *Chakula kimepeanwa kwa watu* badala ya *watu wamepewa chakula.*
4. *Amepeana kalamu kwake* badala ya *Amempa kalamu*

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kwamba umbo la kitenzi 'ku-pa' halimo akilini mwa waneni wengi nchini. Kitenzi hiki kwa wengi ni 'ku-pea'. Hii ndiyo maana -peana haileti maana ya ile kauli ya kutendeana bali inaleta maana ya ku-mpa mtu, kitu, maana ambayo si sahihi kimatumizi.

Hali nyingine inayotatanisha ni katika matumizi ya ngeli ya mahali -ko, na kiwakilishi nafsi cha ngeli ya kwanza **m -,** ambacho ni **yu -**.Kiwakilishi hiki hutumiwa pamoja na ngeli ya mahali ili kuunda maneno kama: **yuko, yumo na yupo.** Baadhi ya waneni wa lugha hii hudondosha kiwakilishi nafsi hicho na badala yake kutumia irabu au vokali ya a – ambayo kwa kawaida hutumiwa katika ulinganifu wa kisarufi wa ngeli ya kwanza. Kwa mfano, sentensi kama hizi hutumiwa kimakosa:

1. *Mama ako kwa nyumba* badala ya *Mama yumo nyumbani*
2. *Ako katika shamba* badala ya *Yuko shambani*

Wakati mwingine pia neno hili -ako hutumiwa badala ya neno 'ana' katika sentensi zinazoonyesha umilikaji wa kitu au vitu. Kwa mfano, sentensi kama hizi huweza kutamkwa:

1. *Yeye ako na gari* badala ya *Yeye ana gari*
2. *Mtoto ako na viatu zake* badala ya *Mtoto ana viatu vyake*.

Katika mifano niliyotoa, ngeli ya KI/VI hutumiwa kimakosa pia miongoni mwa watu wengi humu nchini, hasa wanafunzi wa shule.

Neno jingine linalotumiwa aghalabu katika muktadha usiokubalika, ni neno ati. Kila lugha ina utamaduni wake ambao hujitokeza kupitia waneni wa lugha hiyo. Lugha ya Kiswahili kama lugha nyingine yoyote ina kanuni au nidhamu yake kulingana na jinsi waneni wake wanavyotumia maneno katika miktadha mbalimbali. Iwapo maneno yatatumiwa katika miktadha isiyokubalika, basi wasemaji hao hawajaimudu lugha hiyo ipasavyo. Kama wanavyotueleza Trudgill (1974) na Halliday (1978) ni kwamba lugha hutuonyesha mambo yanayothaminiwa na jamii na kwamba asasi hii huusawiri utamaduni wa jamii hiyo.

Tunaporejelea neno ati tunaona kwamba katika maongezi ya kawaida, neno hili limevuka mipaka ya umri na hadhi iliyowekwa ya jinsi ya kulitumia, na sasa linatumiwa kiholela tu. Neno hili humaanisha kuvuta usikivu au pia huweza kutumiwa kuashiria shaka. Kwa mfano, ikiwa mtu ana shaka juu ya jambo fulani, huweza akalitumia kuonyesha shaka hiyo. Mifano mahsusi ya sentensi ni kama hii:

- Ati umesema nini? (kuvuta usikivu)
- Umeniambia ati nguo hii ni nzuri? (kuonyesha shaka)

Neno hili linapotumiwa katika muktadha unaokubalika hasa kwa kuzingatia kuwa watumiaji wana viwango sawa vya hadhi au umri, huwa halina shaka. Lakini mwelekeo unaoibuka sasa ni kutumia neno hilo katika muktadha na hali isiyokubalika kijamii. Kwa mfano, watoto wenye umri mdogo pamoja na vijana, hawajaelekezwa ipasavyo kuhusu matumizi ya neno hili hasa pale wanapoongea na wakubwa wao. Wakati mwingine utamsikia mtoto mdogo akitamka: *Baba amesema ati umpelekee chakula.* (ikiwa anamwambia nduguye au hata mzazi wake mwingine).

Au katika mazingira ya shule utasikia sentensi kama hizi:

- *Mwalimu amesema ati tumpelekee vitabu,* (ikiwa anawaambia wanafunzi wenziwe).
- *Mwalimu amenituma ati nikwambie ukamwone.* (ikiwa mtoto anamjulisha mzazi wake yale aliyotumwa na mwalimu).

Wale wanaosikia sentensi kama hizi zikitamkwa na watoto, huenda wakadhani kuwa watoto hao hawana nidhamu hata kidogo. Lakini ukweli ni kwamba hawajaelekezwa vyema ili kutambua namna wanavyopaswa kuongea na wakubwa wao.

Mbali na matumizi ya neno hili, kuna baadhi ya maneno mengine pia ambayo maana zao zimechukua mkondo tofauti na ule uliopo. Kwa mfano, neno “ndugu” linazidi kuchukua maana finyu zaidi ya lilivyokusudiwa. Maana ya jumla ni kwamba neno linamhusisha kaka (ndugu wa kiume) na dada (ndugu wa kike). Lakini unapotamka neno hili, fikra za wengi nchini ni kwamba unazungumzia juu ya ndugu wa kiume pekee. Neno ‘kaka’ halimo katika fikra za watu wengi. Hali hii ndiyo Massamba na wengine (2001:27) wanasema kuwa ni kuumomonyoa utamaduni kwani kila lugha ina utamaduni wake unaopaswa kuzingatiwa na wasemaji wa lugha hiyo.

Neno lingine linalochukua muundo-neno tofauti ni “kichochoro” ambacho ni njia nyembamba, hususan inayotumiwa na watu watembeao kwa miguu. Neno hili linapotamkwa “kichocho” kumaanisha kichochoro, huleta maana tofauti kabisa na ile ya njia. Kichocho ni ugonjwa unaomfanya mtu kutoa mkojo wenye damu, maana iliyo tofauti kabisa na ile inayoshikiliwa na wengi, kwamba ni aina ya njia.

Kutokana na mifano michache niliyogusia hapo juu, ni dhahiri kuwa Wakenya wanakabiliwa na daro kubwa kuhusu mkondo unaoibuka wa matumizi ya Kiswahili. Iwapo mambo yaliyojadiliwa hapo juu ni njia moja ya kukuza Kiswahili, basi inatupasa tuchunguze upya namna ya kuikuza lugha hii bila kuvuruga nyenzo za ukuaji wake. Mti hawendi ila kwa nyenzo.

### 1.2 Mapendekezo

Katika makala hii nimejaribu kuonyesha mwelekeo wa matumizi ya Kiswahili nchini Kenya. Nimeonyesha jinsi waneni wa lugha hii wanavyojiundia maneno bila kujali athari za mwelekeo huu, hususan mustakabali wa Kiswahili nchini. Kutokana na hali hii, ninatoa mapendekezo yafuatayo:

- Ipo haja ya kurejelea 'machimbo' ya Kiswahili mlimosaki hazina bora ya msamiati wake wa asili. Shehena hii kubwa imesambaa miongoni mwa waneni wa ndimi za Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti ufanywe ili kufaidi hazina hii ambayo itatoa mchango aali katika kukuza lugha hii kimsamiati.

- Ukosefu wa istilahi sio tatizo la Kenya pekee bali ni tatizo la ulimwengu mzima. Ikumbukwe kuwa kutokana na shida hii, utaratibu wa uundaji istilahi ulianza zamani kupitia kwa mashirika kama lile la *International Standardization Organization (ISO)*, shirika lililoundwa mnamo mwaka wa 1946. Aidha, mojawapo ya sababu za uundaji wa Shirika la *Inter-Territorial Language Committee* mnamo mwaka wa 1930 ni kusanifisha lugha na istilahi katika nchi za Afrika Mashariki. Hali ilivyo sasa nchini Kenya ni ya kutatanisha. Kuzuka kwa istilahi kochokocho zinazokanganya, na ambazo hutumiwa miongoni mwa wasomi na waalimu wa Kiswahili, si dalili ya upeketevu bali ni ukosefu wa ushirikiano ili kuzisanifisha. Katika kutatua tatizo hili, ipo haja ya kujenga ushirikiano hasa kupitia taasisi za Kiswahili nchini Kenya na Tanzania ili kujenga misingi bora ya usanifishaji huo.

- Ikiwa baadhi ya dhana mpya hasa za kiteknolojia hazitaweza kutafutiwa msamiati muafaka katika mazingira na utamaduni wa Kiswahili, basi uundaji wa msamiati mpya ufanywe, lakini kwa kuzingatia misingi ya kisayansi ya uundaji wa msamiati.

- Ipo haja ya Wakenya kujizuia kukimbilia Kiingereza ili kiweze kuafiki mahitaji yetu ya lugha. Tunaweza kujiepusha na ukiritimba wa Kiingereza na badala yake kupigia mbizi bahari ya msamiati mwingi tulio nao katika lugha za kibantu ili kujiafu, na kuipa lugha ya Kiswahili hadhi inayostahili.

- Tahadhari inatolewa hapa kuhusu matumizi ya kiholela ya lugha hii miongoni mwa viongozi kama vile wanasiasa, wazazi na waalimu. Jamii haina budi kutathmini upya mifumo na asasi zake, hususan zile zinazohusiana na elimu ya watoto, ili kuona kwamba lugha yenye nidhamu na inayoheshimu miiko na kaida za jamii inatumiwa.

## Marejeo

Besha, R. (1972): “Lugha ya Kiswahili hivi leo hasa katika siasa” Makala katika *Kiswahili,* Juzuu 42/1, TUKI, Dar es Salaam.

Halliday, M.A.K. (1978), *Language as Social Semiotic,* London, Edward Arnold.

Massamba, D.P.B. na wenziwe, (2001), *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*, TUKI, Chuo Kikuu, Dar es Salaam.

Momanyi, C. (1998), “Sheng”: Ukuaji au Udunishaji wa Kiswahili?” Makala katika *Jua*, Juzuu 2/6, Cologne.

.

Nabhany, S.A. (1978), “ Kandi ya Kiswahili”. Mswada (Haujachapishwa).

Nkwera, F.N.V (1978), *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo,* Dar es Salaam, Tanzania Publishing House.

Prah, K.K. (1993), *Mother Tongue for Scientific and Technological Development in Africa*, Cape Town, ZED.

Trudgill, P. (1974), *Sociolinguistics: An Introduction,* London, Penguin Books.